

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA NANE

31 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA NANE TAREHE 31 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

488. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani kwa Shule za Mwembe – Mbaga, Same na Chome - Suji ambazo hazina Walimu kutokana na mazingira magumu ya kazi.

489. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (LUPA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Watumishi wa Kada ya Afya na Elimu katika Wilaya ya Chunya.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

490. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, lini Serikali itautaarifu Umma kuhusu changamoto za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi ili Waniasia wasipotoshe Wananchi.

491. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani wa dharura wa kudhibiti Mito inayopanuka na kuhatarisha maisha na mali za Wananchi katika Jimbo la Kawe.

WIZARA YA NISHATI:

492. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itakamilisha miradi ya Umeme katika Vitongoji na Vijiji ambavyo havijafikiwa na miradi hiyo Wilayani Karatu.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

493. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itarejesha utaratibu wa *Recognition of Prior Learning*.

494. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kigezo cha mtihani wa kuandika kabla ya kujiunga na Vyuo vya Ufundi (VETA) ni cha lazima kwa Wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

495. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, kuna mpango gani wa kuimarisha upatikanaji wa mtandao wa simu katika Kata 29 za Jimbo la Tabora Mjini.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

496. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga majosho na malambo katika Kata za Bendera, Kalemawe na Maore katika Jimbo la Same Mashariki.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

497. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaanza kuwa na Ofisi ya NIDA na RITA katika kila Halmashauri nchini.

WIZARA YA AFYA:

498. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni kweli kauli ya Serikali ya Hospitali kutozuia maiti kwa sababu ya deni la matibabu ni ya kisiasa.

**499. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE
RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni madhara gani humpata Mtoto anapozaliwa na kuchelewa kulia au kutolia kabisa.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**500. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, kwa nini Serikali isiweke kwenye Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka kipaumbele cha kudhibiti vitendo vya udhalilishaji Watoto Nchini.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA
31 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**